

NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

2 Januari 2016

Kwa Wabaha'i wa Ulimwengu

Marafiki Wapendwa sana,

Tunawaandikia maneno haya kutoka katika mkusanyiko ambako, kwa siku tano mfululizo, Washauri wa Bara wametafakari kwa ari kubwa maana ya Mpango unaofuata wa Ulimwengu. Mashauriano yao yenye umaizi yamechotwa juu ya maono kuhusu mchakato wa ujengaji uwezo ambao unafanyizwa katika maelfu ya klasta ulimwenguni kote. Maelezo mengi yaliyotolewa wakati wa Kongamano hili huthibitisha ubunifu, ushupavu na ukuaji wa uwezo mbalimbali wa jumuiya ya Jina Kuu Kabisa na, zaidi ya yote, utegemeaji wake juu ya mathibitisho ya Mwenyezi Mungu. Kuna utambuzi uongezekao miongoni mwa watu katika sehemu zote za ulimwengu wa uletaji wa matokeo yenye kufaa ya tiba ya Baha'u'llah kwa ajili ya uponyaji wa maradhi ya jamii.

Kabla ya kuhitimisha karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi, hapo kuna kitambo kidogo cha muda ambacho kipo kati ya siku kuu mbili za maadhimisho ya siku za ukumbusho kihusianacho na nyaraka zenye umuhimu usio na kikomo. Kinaanzia na siku kuu ya miaka mia moja ya ukumbusho wa Waraka wa Mpango Mtakatifu uliofunuliwa na Abdu'l-Baha, mara marafiki wanapoingia kwenye hatua mpya katika ukunjukaji wa Mpango huo. Kinaishia kwenye kutimia kwa miaka mia moja tangu Kupaa kwa Abdu'l-Baha, ambao ulifuatiwa na ufunguzi wa Wasia na Agano la Bwana. Wakiwa na fikra hizi akilini, na katika maandalizi kwa ajili ya mashauriano yao, Washauri wa Bara, wakiongozwa na wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, walitembelea nyumba ya Bwana – mahali ambapo tatu kati ya Nyaraka za Mpango Mtakatifu zilikuwa zimefunuliwa na ambapo, majuma machache baada ya kufariki kwa Abdu'l-Baha, Agano Lake na Wasia vilisomwa kwa sauti kubwa kwa waumini kutoka mabara manne. Katika Nyumba ile takatifu, kwenye mkesha wa Kongamano la sasa, vifungu vilighaniwa kutoka zile Hati mbili ambazo, Shoghi Effendi alielezea, zilianzisha mwendo michakato kwa ajili ya uenezaji wa Imani na uanzishwaji wa Utaratibu wake wa Kiutawala. Huu ulikuwa ni utangulizi wa maandalizi kwa ajili ya ushauriano wa siku tano uliolenga juu ya kutawanya kwa mapana zaidi mwanga wa Baha'u'llah na kuimarisha uwezo wa asasi Zake kuwa kama mifereji ambayo kupitia kwayo Baraka Zake zilizoahidiwa ziweze kuwatiririkia wanadamu.

Maelekezo ya Mpango ujao wa Miaka Mitano yamo katika ujumbe ambao tuliutoa kwenye Kongamano hili kwenye siku yake ya ufunguzi na ambao wakati huo huo ulisambazwa kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa. Jitihada kubwa mno ambazo zitahitajika kutoka kwa wapendwa wa Bwana zilitambuliwa kwa udhahiri na Washauri, lakini pia walielezea imani yao

katika uwezo wa ulimwengu wa Kibaha'i kukabiliana na changamoto hii. Kazi kama hiyo itakapokuwa imetafakariwa kwa dhati mapema zaidi, lakini kwa kuzingatia kile kinachofanikishwa katika Mpango wa sasa, nyanja za uwezekano zipo wazi zaidi kuliko wakati wowote hapo awali. Mioyo yetu ilisisimuliwa kwa taarifa ambazo zilianza kuwasili, ndani ya saa kadhaa baada ya kutolewa kwa ujumbe wetu kwenye Kongamano, za marafiki wakija pamoja kwa shauku kubwa katika mazingira ya aina zote ili kusaidiana kuweza kuelewa yaliyomo katika ujumbe huo. Tunatumaini kwamba ujifunzaji wa ujumbe huu utasambaa kwa haraka kwa jumuiya nzima. Wakati huo huo, asasi zitakuwa zinafanya maandalizi yoyote yawayo ya lazima ya kiutawala na kimpangilio ili kuhakikisha mwanzo wenye kheri kabisa wa Mpango kwenye Ridvan.

Katika miezi michache iliyobaki basi, kazi ya Mpango wa sasa, hasa uanzishaji wa program mpya za ukuaji, itaendelea kufuatiliwa. Kila hatua inayochukuliwa katika mwelekeo huo itazidisha utayari wa jumuiya ya ulimwengu mzima kuanza jambo kubwa la kijasiri la miaka – mitano ijayo. Kila kitambo kidogo kina thamani kubwa sana. Tuna shauku kubwa kuona kila muumini akichagua njia ya huduma ya wakfu na jitihada ya hali ya juu ambayo kwayo mara kwa mara Abdu'l-Baha aliwaitia marafiki katika Waraka wa Mpango Mtakatifu. Katika sala zetu za dhati kwa niaba yenu, tutamsihi Mwanzilishi wa Mpango ule kuwaombea mbele ya kiti cha enzi cha Baba Yake ili Aweze kuwaongoza katika huduma yenu ilimradi kuna roho zinazohitaji mkate wa mbinguni.

Nyumba ya Haki ya Ulimengu